ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 45*** ***25th November, 2022***

## *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No 45 Vol.103 Dated 25th November, 2022*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 690 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetengenezwachini ya kifungu cha 29 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MTWARA ("MTWARA WSSA"), YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2022

Jina

1. Amri hii litajulikanakama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara ("Mtwara WSSA") (Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2022.

Bei na ada

2. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mtwara WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza la Amri hii.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitazingatia masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei, ada na malipo yaliyoidhinishwa, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara iwasilishe EWURA, kabla ya tarehe 30 Novemba 2022, vielelezo kuwa

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

imetoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na elimu kwa wadau wake ikiwemo wateja, viongozi wa serikali na dini, wawakilishi wa wananchi na wa jumuiya mbalimbali juu ya utekelezaji wa bei mpya;

(b) ifikapo tarehe 31 Disemba 2022 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

Sura ya 414
TS Na 193/2010

(c) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kifungu Na. 43 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji, na kanuni Na. 6 ya Kanuni za Utaratibu wa Kukusanya Ada na Tozo za Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(d) ifikapo Juni 2024 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara itawasiliana na Manispaa ya Mtwara ili kupata eneo la kutupa majitaka ambalo kwa sasa linaendeshwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara inatakiwa kuchapisha na kusambaza mkataba wake wa huduma kwa mteja na kutoa elimu kwa wateja wake na wadau wengine juu ya mkataba huo na kuwasilisha ushahidi wa kufanya hivyo EWURA ifikapo tarehe 31 Disemba 2022 au kabla ya hapo;

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(g) Mtwara WSSA, kila mwaka na kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hii;

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

(h) Mtwara WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mtwara WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la wateja | Matumizi ($m^3$) | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| Majumbani | 0-10 | 1,110 | 1,785 | 1,896 |
| | >10-20 | 1,280 | | |
| | >20 | 1,400 | | |
| Biashara | 0-10 | 2,030 | 3,100 | 3,300 |
| | >10-20 | 2,210 | | |
| | >20 | 2,440 | | |
| Taasisi | 0-10 | 2,030 | 3,100 | 3,300 |
| | >10-20 | 2,150 | | |
| | >20 | 2,380 | | |
| Viwanda | 0-10 | 2,030 | 3,170 | 3,366 |
| | >10-20 | 2,210 | | |
| | >20 | 2,440 | | |
| Magati | | 1,000 | 1,500 | 1,500 |
| Boza | | 3,510 | 3,721 | 3,944 |
| Wastani | | 1,480 | 2,070 | 2,198 |

Jedwali Namba 1(b): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | |
|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya gharama za maunganisho na nguvu kazi kama | 26,000 | |

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | |
|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| | ilivyobainishwa katika kufungu cha 24 Kanuni za Maji za mwaka 2013. | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | |
|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| Majumbani | 20,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 30,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 30,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 40,000 | 15,000 | 15,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| MAELEZO YA SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA | KIASI CHA FEDHA (SHILINGI) | |
|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 |
| A. Uwekezaji Mpya | | |
| Kujenga choo kipya Mbawala chini | 5,000,000 | |
| Kujenga choo kipya Mnyawi juu | 5,000,000 | |
| Kujenga choo kipya Mnyawi chini | 5,000,000 | |
| Kujenga makazi ya wafanyakazi Mtawanya | 30,000,000 | 20,000,000 |
| Kufanya utafiti wa maji na kuchimba kisima kimoja Mbuo | 49,000,000 | |
| Kufanya utafiti wa maji na kuchimba kisima kimoja Mchuchu/Rwelu | | 45,000,000 |
| Kufanya utafiti wa maji na kuchimba kisima kimoja Mbawala Chini | | 35,000,000 |
| Kufanya utafiti wa maji na kuchimba kisima kimoja Nanyamba | 48,000,000 | 28,800,000 |
| Kufanya utafiti wa maji na kuchimba kisima kimoja Mtawanya | 51,000,000 | 51,000,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| Kununua dira 3300 kwa ajili ya maunganisho mapya | 230,000,000 | 88,000,000 |
| Kununua na kufunga dira kubwa 8 kwa ajili ya maeneo ya uzalishaji wa maji na DMA 11 | 44,000,000 | 48,000,000 |
| Kuanzisha DMA 30 | 120,000,000 | |
| Kununua mabomba ya DN90mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 10 - Nanyamba | 66,900,000 | 66,900,000 |
| Kununua mabomba ya DN63mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 15 - Nanyamba | 37,700,000 | 37,700,000 |
| Kununua mabomba ya DN90mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 8 - Mbawala chini | 44,812,000 | 44,812,000 |
| Kununua mabomba ya DN63mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 10-Mbawala chini | 33,900,000 | 33,900,000 |
| Kununua mabomba ya DN110mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 1 -Mbuo | 9,600,000 | 9,750,000 |
| Kununua mabomba ya DN160mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 15 - Mbuo | | 180,500,000 |
| Kununua mabomba ya DN110mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 10-Mbuo | 78,900,000 | 105,200,000 |
| Kununua mabomba ya DN90mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 10 -Mbuo | 66,900,000 | 66,900,000 |
| Kununua mabomba ya DN63mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 15-Mbuo | 45,360,000 | 68,040,000 |
| Kununua mabomba ya Upvc DN110 PN12 kwa ajili ya kutanua bomba kuu la Naumbu kwa kilometa 8 | 129,340,000 | 64,670,000 |
| Kununua mabomba ya GS DN100mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 2 - Naumbu | 95,000,000 | 47,500,000 |
| Kununua mabomba ya GS DN80mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 3 - Naumbu | 108,499,500 | 54,249,750 |
| Kununua mabomba ya GS DN50mm kwa ajili ya kutanua mtandao kwa kilometa 1 - Naumbu | 15,180,000 | 15,180,000 |
| Kununua viungio kwa ajili ya kupanua mtandao wa mabomba | | 106,000,000 |
| Kujenga kilometa 8 za mabomba makuu Hiari Mkunwa | 104,000,000 | 156,000,000 |
| Kujenga kilometa 8 za mabomba makuu Naumbu | 129,340,000 | 64,670,000 |
| Kujenga kilometa 0.4 za bomba la kusafirisha maji Rwelu | 83,250,000 | |
| Kujenga kilometa 1.5 za bomba la kusafirisha maji Mtawanya | 103,500,000 | 51,750,000 |
| Kujenga kilometa 0.6 za bomba la kusafirisha maji Mbuo | 83,250,000 | 35,000,000 |
| Kuendeleza chemchem mpya Mchuchu-Kipokoso | 200,000,000 | 400,000,000 |
| Kupanua tangi la kutuamisha maji la sasa ili kuongeza uwezo wake maradufu | | 100,440,000 |
| Kupanua uwezo wa kunururisha maji maradufu | 55,800,000 | |
| Kununua pampu 3 za kusukumia dawa | 14,000,000 | 27,000,000 |
| Kununua na kufunga pampu 2 za kuzamishwa kwa ajili ya visima vya Mtawanya | 36,000,000 | |
| Kununua na kufunga pampu 2 za kuzamishwa kwa ajili ya visima vya Mbuo | 28,000,000 | |

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| Kununua na kufunga pampu 3 za kuzamishwa kwa ajili ya visima vya Nanyamba | | 16,000,000 |
| Kununua na kufunga pampu mbili za kuzamishwa kwa ajili ya Mbawala Chini | | 24,000,000 |
| Kununua na kufunga pampu 2 za akiba Mchuchu | | 110,000,000 |
| Kununua na kufunga pampu 2 za akiba Mangamba | 76,000,000 | 76,000,000 |
| Kununua na kufunga vyoyozi 12 | 13,600,000 | |
| Kununua kompyuta 44 | 37,000,000 | 37,000,000 |
| Kununua vifaa vya ofisi | 67,800,000 | 37,000,000 |
| Kununua simu za mkononi kwa ajili ya waendeshaji wa mitambo | 4,500,000 | |
| Kununua vifaa vya matangazo | 6,000,000 | |
| Kununua magari 2 | 160,000,000 | 279,194,333 |
| Kununua pikipiki 9 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| Kununua pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) 3 | 8,000,000 | 8,000,000 |
| Kuboresha huduma ya majitaka Manispaa ya Mtwara | | 1,000,000,000 |
| Kununua magari ya kuondoa majitaka | 290,000,000 | |
| Kununua na kunakili GIS software | 37,000,000 | |
| Kununua GPS software | 6,000,000 | |
| Kununua GIS software | 37,000,000 | |
| Jumla Ndogo | 2,909,131,500 | 3,649,156,083 |
| B. Ukarabati na Kubadilisha Vifaa | | |
| Kukarabati karakana ya useremala | 9,000,000 | 6,000,000 |
| Kukarabati jengo la gereji | 22,500,000 | 15,000,000 |
| Kukarabati karakana ya mabomba | 6,750,000 | 4,500,000 |
| Kukarabati jengo la pampu la Mtawanya | 17,484,855 | 11,656,570 |
| Kulibadili jengo la zamani la pampu la Mtawanya kuwa ghala | 3,375,000 | 2,250,000 |
| Kukarabati vyoo vilivyopo Mtawanya, Nanyamba na Mbawala | 17,460,000 | 11,640,000 |
| Kukarabati nyumba moja ya wafanyakazi Rehabilitation of one staff house at Mangamba | 11,250,000 | 7,500,000 |
| Kukarabati nyumba mbili za wafayakazi Mangamba | 11,250,000 | 7,500,000 |
| Kukarabati magati 20 | 22,275,000 | 14,850,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| Kukarabati tangi la Nanyamba lenye ujazo wa $90m^3$ | 2,700,000 | 1,800,000 |
| Kukarabati tangi la Hiari lenye ujazo wa $315m^3$ | 19,080,000 | 12,720,000 |
| Kukarabati tangi la Mbawala Chini lenye ujazo wa $150m^3$ | 16,380,000 | 10,920,000 |
| Kubadili dira za wateja 3000 | 150,000,000 | 80,000,000 |
| Kukarabati mtandao wa mabomba Mtwara na Nanyamba | 337,937,740 | 232,140,000 |
| Kubadili kilometa 0.4 za bomba kuu Hiari Mkunwa | | 73,200,000 |
| Kukarabati chemchemi ya Mikindani | 110,000,000 | |
| Kubadili pampu 6 za kusukuma dawa | 63,600,000 | 6,800,000 |
| Kubadili kifaa cha kuchanganyia dawa | 10,500,000 | |
| Kukarabati *control panel* 4 Mtawanya | 17,100,000 | 3,600,000 |
| Kukarabati *control panel* 2 kwa ajili ya pampu za kuzamishwa Mbuo | | 11,400,000 |
| Kukarabati *control panel* moja kwa ajili ya pampu za kuzamishwa Rwelu | 5,400,000 | |
| Kukarabati *control panel* 3 kwa ajili ya pampu za kuzamishwa Nanyamba | | 3,600,000 |
| Kukarabati *control panel* 2 kwa ajili ya pampu za kuzamishwa Mbawala Chini. | 5,400,000 | |
| Kukarabati pampu 3 Mchuchu | 18,000,000 | 12,000,000 |
| Kubadili pampu 2 Nanyamba | 99,000,000 | 33,000,000 |
| Kubadili pampu moja Hiari | | 22,800,000 |
| Kubadili komputa 8 | 15,000,000 | 8,000,000 |
| Kubadili samani vipande 30 kama vile viti, meza na makabati | 35,000,000 | 22,000,000 |
| Kubadili vifaa vya ofisi kama vile printa, skana, viyoyozi, na feni | 15,000,000 | 15,191,313 |
| Kubadili komputa moja ya mezani | 2,500,000 | |
| Kubadili pikipiki 8 zilizoisha muda wake | 9,000,000 | 9,000,000 |
| Jumla Ndogo | 1,052,942,595 | 639,067,883 |
| JUMLA KUU | 3,962,074,095 | 4,288,223,966 |

JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Kiashiria cha Utendaji | Uniti | Shabaha ya Utendaji | |
|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 |
| Maunganisho Mapya ya Maji Safi | Idadi | 1100 | 1100 |
| Upotevu wa Maji | % | 27 | 25 |
| Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato (bila | % | 99 | 100 |

*Tangazo la Serikali Na. 690 (Linaendelea)*

| Kiashiria cha Utendaji | Uniti | Shabaha ya Utendaji | |
|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 |
| malimbikizo) | | | |
| Kiasi cha Watu Kilichofikiwa na Huduma | % | 92 | 95 |
| Wastani wa Muda wa Kutoa Huduma | Saa | 22 | 24 |

JEDWALI LA NNE

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| AINA YA GHARAMA | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|
| Uzalishaji wa Maji | 281.91 | 303.15 |
| Umeme kwa Ajili ya Uzalishaji wa Maji | 1,308.70 | 1,411.65 |
| Usambazaji wa Maji | 433.20 | 456.88 |
| Matengenezo | 1,594.16 | 1,635.19 |
| Watumishi | 1,590.01 | 2,865.67 |
| Utawala | 1,345.96 | 1,402.79 |
| Matangazo ya Biashara | 31.68 | 33.21 |
| Matukio na Michango | 58.904 | 59.71 |
| Gharama za Benki na Riba za Mikopo | 12.00 | 12.00 |
| Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo | 6,656.52 | 8,180.25 |
| Uchakavu | 1,655.03 | 1,913.52 |
| Uwekezaji Mdogo | 2,307.04 | 2,374.70 |
| Jumla ya Mahitaji ya Fedha | 10,711.84 | 12,561.72 |
| Ondoa :Mapato Yasiyo ya Mauzo ya Maji | 430.28 | 453.21 |
| Mahitaji ya Fedha Kutoka Kwenye Mauzo ya Maji | 10,281.57 | 12,108.52 |

Dodoma,
24 Novemba, 2022

MODESTUS M. LUMATO
*Director General*